# TARATIBU ZA UTOAJI WA LESENI ZA BIASHARA KATIKA MANISPAA

1. Chukua fomu ya maombi ya leseni za biashara (TFN 211 Business license application form) inayopatikana kitengo cha Biashara;
2. Soma kwa makini na jaza kila kipengele kwenye fomu ambacho kinahusiana na biashara yako. Ni muhimu kusoma maelezo yote yaliyoko kwenye fomu kabla hujaondoka o si ya Biashara ili uweze kupata maelekezo kwenye vipengele ambavyo hujavielewa.
3. Ukaguzi wa maa sa Mipango-miji, Afya na biashara: Ukaguzi hufanywa kwa baadhi ya biashara mfano bucha, nyumba za kulala wageni, migahawa, gereji na mashine za kusaga na kukoboa nafaka.
    - Afisa Afya anakagua na kutoa ushauri wa kiafya kulingana na aina ya biashara inayoombwa.
    - Afisa Biashara anakagua fomu ya maombi ya leseni inayoombwa kama inakubalika kwa mujibu wa sheria ya leseni husika na kama taratibu zote zimezingatiwa.
    - Afisa mipango miji anakagua na kuhakikisha kama aina ya biashara ipo katika eneo stahiki kulingana na matumizi bora ya ardhi katika manispaa.
4. Baada ya mchakato wa maa sa wa Halmashauri kukamilika kwa kuidhinishwa kupewa leseni, muombaji huwasilisha fomu ya maombi iliyoidhinishwa Mamlaka ya mapato Tanzania Mkoa Morogoro kwa ajili ya kufanyiwa makadirio ya kodi na kulipa kwa kadri atakavyoelekezwa na maa sa wa mapato. Hapo hupewa uthibitisho kuwa ameishalipa kodi (Tax Clearance Certi cate) ambao huwasilishwa kitengo cha biashara
5. Utoaji wa Leseni

   Mfanyabiashara huandaliwa hati ya malipo (Bill) kulingana na biashara yake na anailipia benki ya NMB kisha anaandaliwa leseni yake.
6. Muda wa leseni ni miezi 12 tangu leseni inapolipiwa. Baada ya leseni kwisha muda wake, mfanyabiashara anapewa siku ishirini na moja (21) za kulipia leseni yake bila faini, akichelewa atalipia na faini ambayo huanza kwa asilimia ishirini na tano (25%) na huenda ikiongezeka kwa asilimia mbili (2%) kila mwezi
7. Leseni za ushauri na utaalamu maalum pia hutolewa kwa ajili ya kutoa huduma ya ushauri na utaalamu ambapo mhusika ni lazima awe amesomea fani aliyoomba au kuajiri mtu mwenye sifa zinazotakiwa. Huduma hiyo ni kama maabara, wakandarasi mbali mbali, uuzaji madawa, upuliziaji wa madawa ya kuua wadudu (fumigation), huduma za hospitali nk. Utoaji wa huduma hizi mhusika anatakiwa awe amesajiliwa na mamlaka au Bodi za uthibiti wa taaluma husika.

### Huduma/Utaalam na Mamlaka Husika

I. Ukandarasi wa ujenzi- Contractors Registration Board (CRB)
II. Utengenezaji mahesabu/Ukaguzi wa hesabu - National Board of Auditors and Accountant (NBAA)
III. Upuliziaji wa dawa za kuua wadudu kwenye mashamba na majengo - Tropical Pesticides Research Institute (TPRI)
IV. Uwakili - Tanganyika Law Society (TLS)
V. Udaktari - Medical Council of Tanzania (MCT)
VI. Uuzaji madawa, chakula na vipodozi - Tanzania Food and Drugs Authority (TFDA)
VII. Uuzaji wa dawa za binadamu - Tanzania Pharmacy Council (TPC)

8. Ni kosa kisheria kufanya biashara bila kuwa na leseni. Adhabu yake ni kulipia shilingi 50,000 - 100,000 au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote viwili.

### Masharti ya Kuomba na Kupewa Leseni za Biashara

1. Mfanyabiashara anapaswa awe na hati ya usajili iwapo anatumia jina la biashara (Certi cate of Registration or Incorporation)
2. Kama ni kampuni, mwombaji awe na “Memorandum of Article of Association” ambazo inaonyesha kuwa kampuni imeruhusiwa kufanya biashara anayoiomba.
3. Awe na mahali/ eneo linalokubalika kwa aina ya biashara anayoiomba na isiwe vibanda vilivyopo kando kando ya barabara.
4. Mfanyabishara aje na kivuli cha cheti kinachoonyesha kuwa amelipa mapato kwa mujibu wa Sheria (Tax Clearance) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).
5. Masharti mengine ya kupata leseni hutegemea aina ya biashara mtu anayotaka kuanzisha mfano, mgahawa inabidi afuate taratibu zote za afya na kupima wafanyakazi wake.
6. Hati ya Utaalamu (Professional Certi cates) kwa biashara zote za kitaalam.

### Malipo

Kiwango cha ada ya leseni kinatofautina kulingana na aina ya biashara husika. Baada ya ulipaji wa ada hiyo, mfanyabiashara atapatiwa stakabadhi kwa malipo halali ya fedha yake

### Kuhuisha leseni za biashara

Mfanyabiashara anayehuisha leseni anatakiwa aje na nakala ya leseni iliyoisha muda wake pamoja na kibali cha mlipa kodi (Tax Clearence Certi cate) kutoka TRA.

### Wajibu wa Mfanyabiashara

1. Kulipia kila mwaka leseni ya biashara yake kwa mujibu wa makadirio
2. Ni jukumu la kila mfanyabishara kumiliki leseni katika eneo lake la biashara na kuiweka mahala pa wazi ili kuonekana kwa urahisi.

### Faida za Mfanyabiashara kuwa na Leseni ni pamoja na;

1. Kutambulika kama mfanyabiashara halali
2. Husaidia kupata mikopo mbalimbali
3. Husaidia kupata fursa mbalimbali za kibiashara
4. Kuchangia katika uchumi wa Taifa
5. Kuepuka usumbufu wa kufungiwa biashara kwa kutokuwa na leseni halali.
6. Kukua na kuongeza kipato

USAID KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI
VEGA Volunteers for Economic Growth Alliance
iesc THE NONPROFIT THAT MEANS BUSINESS